# PESA MAUA BALI ZAUA

Nchi ya Baraka ilijaliwa maliasili ya kila aina, si misitu mikubwa mikubwa, si_hali ya anga iliyokuwa shwari, si mito iliyokuwa na maji maenge. Wananchi waliishi maisha ya tunu na tamasha. Kilimo kilinoga na kunogea. Mataifa jirani yaliwahusudu. Amani ilidumu_maadamu hakuna yeyote aliyekosa chochote. Habari zisizothibitishwa ni kuwa kando_ya kila barabara, mitunda mingi ilikua, mtembezi yeyote angechuma matunda yoyote, aliyohitaji bure bwerere. Mintaarafu ya hayo, nchi ya Baraka ilipagazwa jina, 'nchi ya_asali kwa maziwa'.

Udongo ulikuwa wenye rutuba. Kutokana na hali hiyo, ilitaniwa kuwa hata ungeangusha kijiti chini kingalimea. Wananchi walikuwa wameshiba siha na kunenepa mithili ya puto lililojazwa hewa. Mungu awape nini awanyime nini?! Licha ya kubarikiwa na Karima nchi ya asali kwa maziwa, tamaa ya pesa iliwanyemelea. Kadri siku zilivyozidi, ndivyo uroho wa kutajirika ulivyowaingia. Mintaarafu ya hayo, walibuni mikakati kabambe ya kujilimbikizia mali na kujaza mifuko. Hatimaye, walipata namna.

"Ya nini kuwa na misitu hii yote ilhali mifuko ni ombwe?" Wenyeji waliulizana kwa utani na utashi. Misitu ilivamiwa kwa fujo. Watu walikata miti kiholela, ungedhani kuwa waliahidiwa zawadi ya thamani kuu wakimaliza kufyeka miti. Wapo waliouza magogo, wengine walipasua mbao, huku asilimia nyingine ikichoma makaa na kuyauza.

"Akili ni mali. Wenzangu, zamani tulikuwa mithili ya chura afaye kiu huku yumo ndani ya kisima", Bwana Puuza alisikika akidai huku ameshikilia shoka, kuendelea kuihujumu miti. Chifu alikuwa miongoni mwa watu wa kwanza waliolalamikia uharibifu huo wa misitu. Aliwatahadharisha kwamba walikuwa wakijiponza. Aliwapa nasaha kuwa, uhaba wa miti ungesababisha uhaba wa vyakula. Hasara ni kuwa alikuwa akimchezea mbuzi gitaa. Wasingeambilika wala kusemezeka.

"Pesa ni mvunja mlima. Mradi uwe na pesa unaweza kununua chochote unachotaka. Ukame ukija, tutanunua vyakula, ushaona?"

Wananchi walijipiga vifua. Wabashiri wa hali ya anga waliandaa vikao kadha wa kadha. Walitoa tahadhari kuwa hali ya anga ingebadilika iwapo ukataji wa miti usingekomeshwa. Licha ya kuwapa hekima, walishikilia kuwa haja yao ilikuwa ni pesa wala sio hali ya anga.

Wanamazingira walijaribu kadri ya uwezo wao kutetea misitu lakini wapi? Walikula mwande. Juhudi zao zilikuwa mithili ya kujaribu kushika nyota angani. Ukataji miti ulikashifiwa redioni, magazetini, kwenye runinga na hata kwenye mitandao ya kijamii. Wananchi walipuuza nasaha hizo. Kauli mbiu kuwa, ukiukata mti mmoja uipande miwili waligeuza ikawa, ukikata mti mmoja, ikate mingine miwili.

Serikali ilijitolea mhanga kupiga marufuku ukataji miti lakini haikufaulu. Walizunguka mbuyu na kuwapiga konde la nyuma walindamisitu. Ufisadi uliwasadifu. Hata mtu aliyehitaji tu boriti moja, angejitoma ndani ya msitu. Kabla ya kupata boriti hiyo angalikuwa tayari ashaiua angalau miti minne, hasara iliyoje!

Mazingira nayo yaliamua kulipiza kisasi kwa kasi. Mvua iliadimika. Vipindi vya kiangazi vilirefuka huku mito ikikauka. Maadamu walikuwa na pesa kama njugu, haikuwa muhali siku za mwanzo. Walimudu kujinunulia vyakula. Hata hivyo, kutoa si kuongeza, chovya chovya ilimaza buyu lao la hazina. Walifilisika. Makali ya njaa yaliwataabisha. Kukawa na ukosefu wa maji. Walikula huu na hasara juu.

Nchi ambayo awali ilikuwa na mandhari ya kupendeza ilibadilika ikawa jangwa. Wananchi waliuma kidole kwa majuto. Nchi yao ya asali kwa maziwa ikawa ya shubiri kwa pilipili. Tamaa yao iliwashikisha tama. Walijuta majuto ya Firauni.